# KUFUNGULIWA KWA MUHURI WA SABA

*Ufunuo 8:1*

*"Na alipoifungua muhuri wa saba, kukawa kimya Mbinguni kama muda wa nusu saa.*

Sikiliza kile Nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo katika siku hizi za mwisho:

Sasa sura ya 8 inafunua tuu mahali ambapo muhuri wa saba unafanyikia ambapo hakuna kitu kingine kinachofunuliwa.

Sasa, hakuna ambacho hakikufunuliwa katika muhuri wa saba.

Sasa, hiyo haina uhusiano wowote na sura ya 7 ya ufunuo. Kule kufunuliwa kwa muhuri wa saba ni kwa kimya kikamilifu. Na kama tuu ningekuwa na muda-Nitajaribu sehemu chache- kuwaonyesha ninyi njia yote tangu nyuma kule mwanzo ambapo muhuri wa saba unazungumziwa. Tangu awali katika kitabu cha mwanzo, huu wa saba- hii mihuri yote iliendelea hata leo.

Sasa, umeona katika kufunguliwa kwa muhuri wa saba, pia uko katika hali tatu za siri. Hiyo moja nitaizungumzia na imezungumza, na hiyo ndiyo siri ya zile ngurumo saba. Zile ngurumo saba kule Mbinguni zitaweka wazi. Itakuwa hasa wakati wa kuja kwa Kristo, kwa sababu Kristo alisema hakuna hata mmoja, atakayejua saa atakayorudi. [1]

Kwa nini, pale hakukuwa, nafikiri, moja ya tatu ya wayahudi wote waliofahamu ya kuwa Yesu Kristo alikuwa duniani. Walikuwa pengine wamesikia juu ya mshupavu wa dini fulani kule chini mahali fulani, lakini hawakuweza kulitilia maanani hilo, waliendelea tu. "Alikuja kwake wala walio wake hawakumpokea. (Yohana 1:11).

Sasa, pale ndio ninaamini hata….. sasa, haikusema Atakuja kwa siri, lakini unyakuo utakuwa ni siri. Kwa hiyo kama pale alipokuja ilikuwa ni siri hivyo, itakuwa ni siri sasa kule kunyakuliwa hakutajulikana. Unaona? Wanataka....Watasema kwa wazi, "Vema niliwaza tungepaswa kuwa na unyakuo kwanza ndiyo hizi hukumu zote zije juu ya dunia. . Atasema, "umesha fanyika tayari, na hamkulijua hilo", itakuwahivyo…… kama vile tu mwizi ajapo wakati wa usiku (Luka 12:37-40; 1 wathesalonike 5:1-3) [2].

Sasa, siri iliyofichika ya Mungu, aliyokuwa nayo kabla ya kuwepo dunia…. Sasa, nyuma kule katika sehemu ya nyuma ya akili ya Mungu, kulikuwa na kitu fulani alichokuwa akijaribu kufanya. Na Alikuwa na kusudi la kufanya hilo, Alitaka aruhusu Yeye mwenyewe aelelezwe. Kwa sababu kwanza, hakukuwa na mwezi, nyota, chembe ya Atomu, wala kipande kidogo cha molekiu au chochote; Yeye alikuwa Mungu. Lakini hakuwa hasa Mungu wakati huo, kwa sababu Mungu ni kiumbe cha kuabudiwa, na hakukuwa na chochote cha kumuabudu Yeye. Kwa hiyo katika akili yake ilikuwa kuu, alitaka hizo sifa/tabia zake zielelezwe. Na katika Yeye kuuliwa na kuwa Mwokozi; ndani yake kulikuwa na kuwa mponyaji. Na hizi sifa zote kuu ambazo tayari tunaziona zikiwa zinaelelezwa tayari, zilikuwa ndani ya Mungu.

Kwa hiyo kwa mawazo yangu, kitu cha kwanza kuumbwa ilikuwa ni Malaika, (Isaya 6:1-4; Waebrania 1:4-14; 2:1-9). Na wao wakamuabudu Yeye na hilo lilimfanya Yeye kuwa Mungu na alianzia kutoka hapo…. Na sasa, wakati Malaika walipoanza kumuabudu Yeye hapo ilikuwa kabla hakujawa na chembe ya molekiu duniani; hakukuwa na chochote. Ilikuwa ni giza; hakukuwa na jua, au mwezi wala nyota wala chochote; hapo sasa alikuwa Mungu. Kama alivyomuuliza Ayubu, ulikuwa wapi nilipoweka misingi ya dunia? Wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, wana wa Mungu walipopiga kelele za shangwe?" unaona? Ulikuwa wapi? Unaona? Hiyo ilikuwa nyuma pale kabla ya dunia (Ayubu 38:4-7).

Sasa, Mungu alikuwa na kusudi na kusudi la siri lililofichika. Na hilo ndilo ninalotaka kuzungumza na kanisa; Siri ya Mungu iliyofichika ambayo alikuwa nayo akilini mwake kabla ya dunia kuanza na jinsi ilivyojifunua mwenyewe kuanzia nyuma kule mpaka saa hii tunayoishi. Unaona? Hapo sasa utaelewa vizuri na kuendelea, naamini kile kinachofanyika.

Siri kuu ya Mungu ya….. Ni siri. Aliiweka iwe siri. Hakuna hata mmoja aliyejua chochote juu ya hilo; hata Malaika hawakuelewa hilo. Unaona? Hakuifunua hiyo. Hiyo ndiyo sababu chini ya ile siri ya saba, wakati muhuri wa saba ulipofunguliwa, kulikuwa na kimya (ufunuo 8:1)

Yesu alipokuwa hapa duniani, walitaka kujua nilini angelikuja. Alisema, " bado siyo---- Hata mwana mwenyewe hajui itaenda kutokea lini" (Matayo 24:36; Marko 13:32). Unaona. Mungu alikuwa nalo hilo mwenyewe ni siri. Na hiyo ndiyo sababu kulikuwa na kimya Mbinguni kwa muda wa nusu saa. Na ngurumo saba zikatoa sauti zao, na Yohana hata alikatazwa kuandika hilo, (Ufunuo 10:1-4) kule kuja kwa Bwana.

Hilo ndilo jambo pekee ambalo bado hajalifunua bado,jinsi Yeye atakavyokuja,na ni lini atakuja ni jambo zuri kwamba Yeye halifunui. Hapana. Amelionyesha kwa kulifunua hilo kwa mifano mbalimbali na ulinganishi katika Biblia.

Kwa hiyo, Biblia yote ni Ufunuo wa siri ya Mungu ndani ya Kristo. Biblia yote inaeleleza, lengo la Mungu alilokuwa nalo; na kusudi moja, ambalo alitaka kulitimiza katika Biblia yote, na matendo yote ya waaminio, katika Biblia ilikuwa ni mfano na ikieleleza lile lengo kuu la Mungu lilikuwa nini. Na sasa katika siku hizi za mwisho Amefunua hilo na kulionyesha hilo. (1korintho 2:6-16). Na kwa msaada wa Mungu, tutaliona hilo hapa asubuhi ya leo. Kile Bwana alichokuwa nacho katika Akili zake na amekidhihirisha.

Kwa hiyo, utaona, ile maana kuu ya kile kilichokuwa kujua hili na kujaribu kulileta kwa watu. Unaona? Na halafu siyo una------- sijaenda kuelezea kindani na kujaribu kulielezea hilo kama Mungu alivyolifunua kwangu. Unaona? Alikuwa anafanya nini?….. anajitambulisha mwenyewe kwa hawa mitume kuwa manabii wote, na zaburi zote, na kila kitu ilikuwa ni Yeye akielelezwa (Luka 24:25-47)

Yeye ndiyo kiini kikuu cha Biblia yote. Kama utasoma Biblia na humuoni Kristo katika kila mstari wake, rudi nyuma na uusome tena. Unaona? Kama huwezi kumuona Kristo katika kila mstari wa Biblia, hapo usome tena huo, kwa sababu umekosa kitu fulani. Biblia ni Kristo. Yeye ni Neno unaposoma, "Hapo mwanzo Mungu aliumba…." Hapo ni Kristo (Yohana 1:1-4). Unaona? Kutoka hapo mpaka "Amen" ya Ufunuo ni kila Neno linamshuhudia yesu Kristo [3]

Na haya mambo ambayo tunayazungumzia yalikuwa yafunuliwe katika siku za mwisho. Kabla tu ya ile tarumbeta ya mwisho, katika wakati wa kumalizika kwa ujumbe wa wakati wa kanisa la mwisho. Hiyo ni sawa. Kama unataka kusoma hiyo sasa, unaweza kugeuza kwa…… nilikuwa tu nimenukuu kwenu usiku wa jana mara mbili au tatu, Ufunuo 10:1-7: "Na katika siku za sauti ya Malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu; hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa na kufunuliwa". Na kuna kitu kimoja tu kilichobakia wakati hiki kitabu cha mihuri saba kitakapofunguliwa, hapo siri yote ya Mungu, kwa nini, ambayo tumebahatisha miaka hii yote, na kutokana na maandiko hakukuwa na namna ya kuielewa mpaka wakati huu wa mwisho, kwa sababu ilikuwa imefichwa. Tumeona alama yake (Ishara), kile ilichokieleleza, lakini haikufunuliwa kwa usahihi mpaka siku hizi za mwisho. Unaona? Sasa, tunapaswa kuwa pale wakati huo wa mwisho.

Sasa kumbuka, na sasa usisahau kuwa hafanyi jambo mpaka kwanza amelifunua hilo; na usisahau pia, kwamba analifanya katika hali rahisi sana kiasi kwamba wenye hekima na akili wanalikosa hilo. Sasa kama unataka uliandike hilo ni katika Mathato 11:25-26. [4]

Sasa tunaenda kufungua sura ya nane ya Ufunuo 8:1. na Mungu wa mbinguni atusaidie sisi, ndiyo maombi yangu. Tunapaswa tukumbuke kuwa huu muhuri wa saba ni mwisho wa mambo yote. Hiyo ni sawa; ni mwisho wa dunia inayohangaika. Ni mwisho wa mahangaiko ya vitu vya asili. Ni mwisho wa kila kitu pale ni mwisho wa baragumu. Ni mwisho wa vitasa. Ni mwisho wa dunia. Ni mwisho hata wa wakati. Wakati unaenda kwisha Biblia ilisema hivyo.

Ufunuo sura ya 10 na mstari wa 1 hadi mstari wa 7. wakati unaenda kwisha Malaika alisema, "Hakutakuwa na wakati tena", wakati hilo---- katika siku za jambo hili kuu litakapotokea. Kila kitu kinaenda mwisho, wakati wa mwisho wa huu muhuri wa saba.

Angalia ni mwisho wa wakati wa kanisa. Ni mwisho wa mihuri saba. Ni mwisho wa baragumu. Ni mwisho wa vitasa, na hata kuishia katika kuanza kwa utawala wa miaka elfu moja hayo yako katika muhuri wa saba.

Ni kama vile kuwasha roketi iende hewani, na hiyo roket inalipuka hapa, na inapopanda juu, halafu inalipuka tena. Inakuwa sehemu 5 vinyota na moja ya hivi vinyota inalipuka na kutoa vinyota vitano tena; na halafu moja ya hivi vinyota inalipuka, na kuvunjika na na kutoa vinyota tena kutoka hiyo halafu; na kuendelea kuishia.hivyo ndivyo ulivyo muhuri wa saba; unamaliza muda wa dunia, unamaliza muda wa hiki na kile. Ina maanisha muda wa hiki na kile. Inamaliza muda wa hiki. Inamaliza muda…. Kila kitu kinaishia tu katika muhuri wa saba.

Sasa, ataenda kulifanyaje? Hicho ndicho tusichojua si ndiyo? Hatujui. Ni wakati wa haya mambo yote, na kuingia katika utawala wa miaka elfu moja.

Angalia kuvunjwa kwa huu muhuri ilikuwa ni jambo kuu sana kiasi kwamba mbingu zilinyamazishwa/shangazwa kwa ukimya wa Nusu saa. Sasa, ni kuu hilo? Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni unyamavu: Mbinguni. Hakukuwa na kitu kilichoendelea kwa muda wa nusu saa.

Sasa, muda wa nusu saa unaweza usiwe mrefu kama una wakati mzuri. Lakini katika hali ya hatari kati ya kufa na kuishi, inaonekana kama ni miaka elfu moja. Ilikuwa ni kuu sana, Yesu kamwe hakulitaja: hakuna hata wote waliobaki Yohana hakuweza hata kuliandika. Hapana. Alikatazwa hapo asiliandike. Unaona; kulikuwa na …. Alikuwa…. Hakuliandika hilo lakini ilikuwa ni kimya tu.

Na wale wazee ishirini na nne ambao walisimama mbele za Mungu pale wakipiga vinubi vyao, waliacha kuvipiga (ufunuo 5:8). Malaika wakanyamaa mbinguni na kuacha kuimba. fikiria, makerubi na maserafi, ambao Isaya aliwaona katika hekalu walikuwa na seti sita…. Au seti tatu za mabawa, matatu juu—mawili walifunika nyuso zao, na mawili juu ya miguu yao, na wakiruka (Isaya 6:1-4). Na usiku na mchana wako mbele za Mungu, wakisema, "Mtakatifu, Mtakatifu, Matakatifu, ni kwa Bwana Mungu mwenyenzi". Na hata walipotembea mle hekaluni au walipoingia hekaluni misingi ya vizingiti vya hekaluni vilitikisika. Na maserafi hawa watakatifu walinyamaa. Malaika wakaacha kuimba. Wakiruka uweponi pa Mungu, wakiimba, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu….. walinyamaza.

Hakukuwa na malaika walioimba, hakukuwa na nyimbo za sifa, hakukuwa na huduma madhabahuni, hakukuwa na chochote kulikuwa na kimya,/utulivu. Ukimya mkuu mbinguni kwa muda wa nusu saa. Majeshi yote ya mbinguni yalinyamaza kwa muda wa nusu saa, wakati siri hii ya muhuri wa saba katika kitabu cha ukombozi ilipovunjwa na kufunguliwa. Fikiria hilo; lakini imefunguliwa. Mwana kondoo anaivunja. Unajua nini?

Walishikwa na hofu (uchaji) ya huo, ninaamini. Hawakujua. Iko pale; walisimama. Kwa nini? Ilikuwa nini?

Sasa hakuna hata mmoja wetu ajuaye; **Lakini nitaenda kuwaambia ufunuo wangu juu ya hilo.** Na sasa mimi sijachukuliwa na uzushi. Kama niko hivyo mimi sielewi hilo. Mnaona? Mimi sijachukuliwa kuangalia vitu kiupandepande au uzushi na mambo ya kuwazia. Nimesema vitu kadhaa ambavyo vinaonekana ni vigeni kwa baadhi ya watu. Lakini wakati Mungu anapokuja hapa na kulithibitisha hilo na kusema ni kweli, hapo sasa hilo ni Neno la Mungu. Inaweza kuonekana ni geni kwa njia hiyo. Unaona?

Na sasa, kwa uhakika ilivyo kwamba nimesimama usiku wa leo hapa mimbarani. **Nilikuwa na ufunuo ambao umefunua……. Uko katika migawanyiko mitatu.** Ambayo **nitawazungumzia sehemu moja kwa msaada wa Mungu.** Hebu twende hapa kwanza. Ufunuo ni huu hapa kwa kuanzia ni….. Nataka ni waambie ni kitu gani. Kilichotokea ni kuwa ngurumo hizi saba ambazo amezisikia zikinguruma na akakatazwa asiziandike. **Hizo ndizo ambazo zinaishikilia hiyo siri, ikiwa iko nyuma ya hizo ngurumo saba zilizo fuatana zikilia.**

Sasa,kwa nini? Hebu tuthibitishe hiyo.Kwa nini? Ni ile siri ambayo hakuna ajuaye lolote juu ya hilo.Yohana alikatazwa asiandike juu ya hiyo,hata kuandika alama juu ya hiyo (Ufunuo10:3-4). Kwa nini? Hii ndiyo sababu hakukuwa na na shughuli yoyote mbinguni;ingeitoa hiyo siri .unaiona hiyo sasa? Kama ni kubwa hivyo,ni lazima iwe imeandikwa.kwasababu ni lazima itaenda kutokea, lakini wakati ngurumo saba…… .[1]

Na kila wakati,ninyi ambao mnachukuwa kanda na kusikiliza,ni natumaini na kutegemea kwamba mmekuwa na ufahamu wa kiroho na kile ambacho Mungu alikuwa anajaribu kukileta kwa watu wake bila kukisema kwa dhahiri.unaona? ni **kitu wakati mwingine….Tunazungumza vitu kwa namna ambayo,inaweza kupunguza watu, kuwafanya wengine waondoke, waendezao,na wengine wazidi kuchimba ndani.Lakini hayo yanafanywa kwa makusudi.lazima ifanywe hivyo.**

Halafu itawafanya wengine waseme, "Mungu unamaanisha anaweza akusudie afanye jambo kama hilo? Hakika amefanya.na bado anafanya. Siku moja alisema, wakati akiwa na maelfu waliomzunguka;Alisema,msipokula nyama ya mwana wa Mungu,Mwana wa Adam, na kunywa Damu yake,hamna uzima ndani yenu"(Yohana 6:53-66).

Ni maneno/kauli ya namna gani hiyo, kwa mtu ambaye alikuwa na huduma kama aliyokuwa nayo? Kwa nini,angeweza kusema, "kula nyama"? huyo ni mla watu.kunywa damu ya binadamu,ni kizuu,kwa maneno mengine,alikuwa anataka tuwe wala watu na vizuu"na kundi lote wakaondoka wakamwacha.

Na alikuwa na baraza la wahudumu waliokuwa pamoja naye,la wale sabini ambao aliwachagua.Na aliwageukia na kusema, utafikirije mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa kutoka huko alikokuwa kwanza? Sasa,hakulielezea hilo,kamwe hakulielezea ni kwa namna gani.Paulo alifanya hivyo baadaye alilisema hilo.Unaona? na halafu wakati hili……..Alisema,utasemaje kwa hawa wahuduma wakati wanamwona Mwana wa Adamu akipaa juu kutoka huko alikotoka? [5]

Na ninafikiri mbinguni ni mahali ambapo mama yangu alizoea kunieleza.Naamini kanisa limekuwa kutoka hapo kufikiri kwamba ilikuwa…..Ni miaka mia moja au mbili iliyopita.nafikiri wale watu wa zamani walizoea kufikiri kuwa kila aliyekufa alienda mbinguni.na alikuwa na kinubi.sasa walijua kuna mahali panaitwa mbinguni,lakini wali……kama hiyo ni hivyo,wanamuziki wote wataipata juu yetu.unaona? lakini siyo mahali kama hivyo.Siyo kupiga kinubi hata kidogo.Siamini kama biblia inafundisha hivyo.Lakini hayo yalikuwa ni mawazo ambayo walikuwa nayo kabla ya ukamilifu wa Neno kuja au kufunguliwa kwa mihuri saba ambayo aliahidiwa kwetu katika huu wakati.Kwamba sasa tutaelewa,naamini kwamba mbinguni ni mahali halisi tu kama hapa palivyo mahali halisi,kwa maana Mungu alituanzia mahali pa katika ukuaji wetu wa kiroho.na ninaamini mbinguni ni mahali halisi kama hapa,ambapo hatukai hapo milele na kukaa tu hapo juu ya mawingu.

Unashangaa kwa nini ulifanya hivyo.lakini baada ya muda unakuwa, kama mkristo aliyekomaa,halafu unalielewa hilo unaona? Kuna kitu fulani kinatuinua juu na unaona kwa nini unapaswa kulifanya hilo.Kuzaliwa kwako kwa kimwili kunaeleleza kuzaliwa kwako kiroho.Jinsi vilivyolingana na wewe,katika maisha haya kadri ulivyokuwa unakuwa,kuna kitu kilikaa vizuri kwa sababu ulitengenezwa kwa ajili ya hilo. (2Petro3:18)

Haikuwa ni kitu cha ajabu usiku ule ulipotatizika mpaka ulienda kanisani.katika mkutano ule,au lile kanisa dogo mahali fulani kwenye kona,ni kitu fulani, na ukaanguka tu madhabahuni? unaona,unaona?Mungu alijua hilo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia (Waefeso1:4) Unaona? Ilionekana ni geni kwako ulifanya hivyo wakati huo lakini sasa unaelewa. [6]

Angalia, angalia hapa, kulikuwa na mnada wakati mmoja na walikuwa na zeze la zamani.mmelisikia hilo mara nyingi,zeze hili la zamani (la kizungu) na mtu wa mnada akauliza nitapewa thamani gani kwa hili? Na wakalichukuwa lile zeze; halikuonekana kama ni kitu sana; lilionekana kitu ovyo, kwa kila kitu hakuweza kupata hata makadirio juu ya thamani yake hatimaye nafikiri alipata thamani ya dollar au kitu kama hicho.

Sasa alikuwepo mmoja ambaye alisimama pale ambaye aliwaza lisingeuzwa hivyo kwa hiyo alienda akalichukuwa akaanza kuliweka mikononi na akaanza kulipigia wimbo na alipofanya hivyo, kila mmoja alianza kulia hawajasikia wimbo huo maishani hata.

Halafu yule mnadi akasema,nitapewa thamani gani? "Elfu mbili" "Elfu tano" "Elfu kumi" unaona? Ni nini? Mkono wa Bwana umefunua kile kilichofichwa ndani ya chombo hiki cha zamani.

Kadhalika hata sasa, kitabu kile cha zamani, kilicho paruzika, kimekuwa kikichekwa, kuchomwa moto, kilifanyiwa dhihaka.lakini wakati unakuja ambapo wana mnada wakidhehebu,Baraza la makanisa duniani,wanakiuza kama ni biashara isiyo na mwenyewe.kuna mnadi wa dhehebu anayekuja.

Lakini kumbuka kuna kitu fulani kilicho ahidiwa katika kitabu hiki cha zamani, ya kuwa kuna aliyekusudiwa kimbele, aliyewekwa wakfu, ambaye sikumoja atakuja, ambaye atakichukuwa na kulifanya Neno la kitabu hiki, lifike kwenye mioyo iliyokusudiwa kimbele, kwa kazi ile ambayo kilitengenezewa, kufunua ahadi ambazo ziko pale ndani. Kinaweza kuonekana cha zamani kama kundi la kizamani la watakatifu wanaovingirika au kitu fulani kingine; lakini inachukuwa mkono wa Bwana, Neno ndani pale, kufunua lile Neno; na inakuwa zaidi kama mtakatifu- anayevingirika. Imekuwa hivyo kwa kila mmoja wetu, si ndiyo, marafiki? Siyo kundi la wazushi inategemea ule upinde wa zeze uko mkononi mwa nani. [5].

Mnamuona Yeye sasa katika Neno na katika Neno lake lote likifanywa dhahiri hapa mbele zetu? Oh kanisa la Mungu aliye hai, amka usingizini usonge mbele: Mwamini Yeye na vyote vilivyo ndani yako. Shikilia kile kwenye kile kigurudumu kidogo katikati ya gurudumu. (Ezekieli 1:15-21).
Hebu hiyo iwekee nanga kila hatua yako na kila mwendo wako unaoufanya.kila wazo ulilonalo,hebu litawaliwe na hiyo nguvu iliyoko ndani yako,**kwa sababu Mungu ameketi hasa katika Neno lake la saa hii katika nuru ya jioni akiionyesha nuru.**

Kila mfano, kila kitu tukienda kwenye mambo ya asili; kwenye Biblia, kwenye sanamu ile aliyoiona Danieli na mfalme wa siku ile,wote waliiona na mambo haya yote. Kila mtu, kila namna, kila hatua, kila mahali katika mwili,vinatuonyesha mahali tulipo katika saa hii hasa unayoishi.hakuna uamsho mwingine utakaokuja juu ya huu. Tulikuwa na uamsho wa kuweka msingi,Luther, kulikuwa na uamsho wa mikono ,upendano,Wesley,upendo….hakukuwa kamwe na huu kama inafundishwa kuwa uamsho wa Wesley, walituma wamisionari dunia yote,moja ya uamsho mkuu sana ambao ulifanywa katika wakati kabla ya huo,halafu ukaja wakati wa Pentekoste, halafu vikaja vidole tofauti tofauti na vitu kama hivyo, wakati wa pentecoste wakati wa ndimi,na pua,na kadhalika.sasa tuko kwenye macho,itasaidia nini kuwa na macho au kutaka nuru,halafu hakuna jicho la kuonea? unaona?lazima kuwepo macho ili uweze kuona. Na sasa hilo linapokuja. Akafungua mihuri saba na akafunua nuru ya wakati wa jioni, akichukuwa siri zote zilizokuwa zimefichika kote huko katika nyakati zote za kanisa na sasa anazifunua kama alivyoahidi kufanya (Ufunuo10:1-7) Tuko hapa leo tukiwa tumekaa katikati ya Neno na Neno likiwa linafunuliwa kwetu na Yesu Kristo kwa hiyo hili ni Neno la Mungu [7]

Bwana wetu alipokuwa hapa duniani,wanafunzi walimuuliza Yeye na kusema, Je Bwana ni wakati huu utakapo warudishia wa Israel ufalme wao(Matayo1:6-8)

Na Yesu akasema, "si kazi yenu kujua nyakati wala majira" "na hakuna hata mmoja atakaye jua, kasema hata Mwana, bado alikuwa hajui"lakina baada ya kufa kwake, kuzikwa na kufufuka, na kupaa utukufuni alipokea kutoka kwa Mungu vile kanisa litakavyokuwa siku za baadaye halafu akarudi tena ili kuleta huu ujumbe kwa kanisa, na ujumbe huu wa kuja kwake na hali ya kanisa itakavyo kuwa nyakati zijazo asingeweza kufanya hivyo kabla ya kufa kwake, kuzikwa na kufufuka, kwa sababu, alikuwa hajajua hilo bado Lakini uliona vile maandiko yanavyosema hapa? Ufunuo wa Yesu Kristo aliopewa na Mungu…(Kristo)

Jinsi ambavyo Baba Mungu amempa Mwanaye Yesu Kristo Ufunuo na yeye akamtuma malaika wake kwa Yohana kuthibitisha mambo yaliyokuwepo, yaliyokuwa, na yatakayokuwa Oh imewekwa vizuri sana Ufunuo 1:1-2 [8]

Lakini hii ni huduma yangu, kuwa amenipa kipawa na kile kipawa ni kuliamsha kanisa kulileta kwenye utambuzi wa kule kuja kwa Kristo, kule kurudi kwa Roho wa Mungu katika kanisa. Liko juu yenu, Roho yule yule Inaweza isiwe kipawa kile kile, lakini Roho yule yule kuna uthibitisho wa aina tofauti, lakini ni Roho yuleyule wakati wote, Roho Mtakatifu uliye naye, ni Roho Mtakatifu niliye naye, ni Roho Mtakatifu tuliye naye sote sisi wote ni watoto wa Mungu [9]

Huduma yangu ni tofauti na huduma ya mchungaji au mwalimu mimi siyo na nikisema kitu kimakosa, ndugu, nisameheni mimi simaanishi hivyo lakini hii ni huduma yangu kumtangaza Yeye, kwamba yuko hapa. [10]

Na kwa hiyo alizungumza na mimi akisema, mihuri saba itaenda kufunuliwa, zile siri saba,zili siri saba katika Biblia zilizo katika mafungu saba ambazo zilikuwa zimefungwa tangu kuwekwa misingi ya dunia itaenda kufunuliwa" na bado sisi ni kundi dogo la watu wanyenyekevu ukilinganisha na dunia yote, tumefurahia hizi baraka na kusikia hizi siri, ndoa na talaka, uzao wa nyoka, na maswali haya mengineyo tofauti ambayo yamefunuliwa kwetu kikamilifu, siyo na mtu lakini na Mungu mwenyewe, ambaye amefunua hizi siri saba za vile kanisa lilivyo kuwa, vile lilivyokuwa ndani ya Kristo pale mwanzoni, na vile ambavyo litafunuliwa siku ya mwisho.

Kumbuka tazama kile ambacho tunaona katika siku hii ya leo ile nguvu ya kuhuisha imekuja kwetu kufungua ile mihuri saba Ilikuwa ni nini? Akili ya mwanadamu? Hapana ile nguvu ya kuhuisha ya Mungu.Unaona? nguvu ya kuhuisha ikizungumza kuwa hili litafanyika. Unaona? Lakini

nguvu za kuhuisha za Mungu ziliifanya dunia ikashuhudia kuwa ni kweli. Na katika hilo, hawakujua ni nini na sisi ambao tunaangalia tu upande huu…….**na ni Bwana wetu juu pale. Unaona? ndiye Yeye aliyefungua mihuri; Yeye ni ile mihuri**,kwa maana Neno kamilifu la Mungu ni Kristo,**na Kristo ni hii mihuri ambayo ilifunguliwa.ni nini kule kufunguliwa kwa mihuri saba? Kumfunua Kristo na hasa wale malaika saba ambao waliwakilisha yale makanisa saba yote yalikamilika**,na hatukuweza kuliona hilo.wakachukuwa picha yake, siyo sisi na yule pale amesimama, hakimu mkuu akijionyesha Yeye ni Alfa na Omega, Yule Mwanzo na Mwisho ni utambulisho wa namna gani?

Vema, kama utageuza ile picha kama hivi na kuangalia (na pengine unaweza kuiona kutoka ulipo kwenye kusanyiko,)ni Kristo.Unaona macho yake yakiangalia kikamilifu kama yawezavyo kuwa, akivalia kifuniko cheupe cha Mungu Mkuu na hakimu wa mbingu zote na dunia! Unaweza ukaona macho yake, pua, mdomo wake? Yeye ni hakimu mkuu; hakuna mwingine zaidi ya Yeye (Ufunuo1:12-16).Na hiyo ni kitambulisho kikamilifu tena, uthibitisho wa kuwa huu ujumbe ni wa kweli ni kweli. Na kumfanya Yeye,sio nafsi ya tatu, lakini ni Yule aliye nafsi ya pekee na nywele nyeupe……….

Nguvu ya kuhuisha ilifanya hivyo kwetu nguvu ya kuhuisha hebu tuone kule kuja kwake nguvu iliyotunyakuwa kutoka mauti kuingia uzima.

Nukuu za kiingareza:

[1] Ule muhuri wa saba kitabu cha mihuri uk,536/575/555-557
[2] Ule muhuri wa tatu kitabu cha mihuri uk.238
[3] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk.16-19
[4] Ule muhuri wa pili kitabu cha mihuri uk.187
[5] Kufunuliwa kwa Mungu Aya 22-26/347-352
[6] Mambo yale yatakayokuwa Aya 40-42
[7] Kristo akifunuliwa katika neno lake aya,161-162
[8] Ufunuo sura ya kwanza (60-1204m). aya.80-84
[9] Usiogope(b2-0620) .Aya E-85
[10] Kutoka wakati huo (62-0713),aya E-102
[11] Kule kuchomoza kwa jua uk. 2/45

---

jiwe la kiroho la kujengea na. 179 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306.

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*